

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA SITA

02 MEI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA SITA – TAREHE 02 MEI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

198. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali italipa kiinua mgongo kwa Wazee ambao hawajawahi kuajiriwa.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

199. MHESHIMIWA KATANI AHMED KATANI (TANDAHIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kumalizia ujenzi wa Sekondari zilizojengwa na Wananchi Kata za Mnchimbwe, Kwanyama na Litehu.

200. MHESHIMIWA DKT. JOSEPH KIZITO MHAGAMA (MADABA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini hoja za ukaguzi hutokea pale fedha za Mfuko wa Jimbo zinapotumika kwa Wajasiriamali.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

201. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kuna mpango gani wa kurudia ujenzi wa Barabara ya Mwigumbi – Maswa ambayo imejengwa chini ya kiwango na imeshaharibika.

202. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itapanua barabara ya Tegeta kuelekea Kiwanda cha Saruji Wazo.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

203. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini umeme utafungwa kwenye Mnara wa Halotel uliopo Kata ya Ngujini Wilayani Mwanga.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

204. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaipatia gari Ofisi ya Zimamoto ya Wilaya ya Igunga.

205. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za kumalizia ujenzi wa Gereza la Chunya.

WIZARA YA KILIMO:

206. MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa pembejeo Wakulima wa Mbogamboga nchini.

WIZARA YA NISHATI:

207. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji na Vitongoji vya Mkoa wa Kilimanjaro ambavyo havina huduma ya umeme.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

208. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Serikali itaanza kutengeneza Bajeti kwa jicho la Jinsia.

WIZARA YA MAJI:

209. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia maji Vijiji vilivyopo Mwambao wa Ziwa Nyasa.

**210. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA
(KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa maji wa Kihesa Mgagao, Masege hadi Masalali - Kilolo.

**211. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI
(MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria Kata za Ikunda, Mwakata, Menga, Shilela na Lunguya - Msalala.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA
02 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**